**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Sita – Tarehe 15 Septemba, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Taarifa ya Serikali kuhusu mtumishi wa Serikali kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kupitia Kitengo cha Benki ya Damu.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Taarifa ya Serikali kuhusu mtumishi wa Serikali kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kupitia Kitengo cha Benki ya Damu.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

104. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu ya nane imekuwa ikijitahidi sana kuweka jiji la Zanzibar katika usafi hasa kwenye maeneo ya mji.  Hata hivyo, zipo gereji bubu na magari mengi mabovu yaliyozagaa katika mitaa na barabarani hali inayopelekea kuharibu haiba ya mji wa Zanzibar.

(a) Je, ni hatua gani ambazo Serikali imepanga kukabiliana na hali hiyo ya uchafu katika mji.

(b) Kwa kuwa Serikali haipendezewi na uharibifu huo, Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi maeneo ya kuweka gereji bila ya kuchafua mazingira ya mji.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji**

135. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali ina mipango mizuri ya kuwaendeleza wajasiriamali wa Zanzibar. Hata hivyo, vikundi vingi vya ujasiriamali vya wananchi wa vijiji vingi vya jimbo la Pandani hawajafaidika na mipango hiyo.

(a) Je, mara ngapi Serikali imetoa elimu, utaalamu, na mafunzo ya ujasiriamali kwa watu wa jimbo la Pandani.

(b) Je, Serikali inazingatiaje na kutekelezaje mahitaji ya mbolea, masoko, pembejeo, dawa, kufungasha, kuchapa (brand), na kusajili kazi za wajasiriamali.

(c) Je, ni zipi juhudi za Serikali katika kuwasaidia vijana wa vijijini kupata elimu ya michezo kama biashara, ajira na ujasiriamali.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

30. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Timu za mpira wa miguu za Zanzibar kama vile Small Simba, Malindi, "Black Fighters" na Ujamaa kwa upande wa Kisiwa cha Unguja pamoja na Chipukizi, Jamhuri na Mwenge kwa upande wa Pemba zilikuwa tishio katika tasnia ya soka hapa Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla katika miaka ya themanini. Na kwa kuwa kuanzia mwanzoni mwa miaka ya elfu mbili hadi leo hii timu zetu na soka letu hapa Zanzibar limeanguka kwa kiwango kikubwa na hatimae timu zetu hizo kupoteza kiwango chake na nyengine kufa kabisa kisoka.

Je, ni sababu gani za msingi zilizolifanya soka letu kuanguka kwa kiasi kikubwa namna hiyo.

150. MHESHIMIWA MOH'D MGAZA JECHA (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Wananchi wa jimbo la Mtambile wanaipongeza Serikali kwa kuanzisha uwanja wa mpira wa miguu wa Wilaya ndani ya jimbo hilo ambao umekabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya na kuanza kutumika pasi na kukamilika ujenzi wa baadhi ya vitu vikiwemo vyoo.

(a) Je, uwanja huo utakamilika lini.

(b) Je, ni tasisi gani itakayoshughulikia uendelezaji wa ujenzi wa vitu vilivyobakia.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

21. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kuleta na hatimae kutegemea dhana ya uchumi wa buluu kama chanzo kikubwa cha mapato ya nchi. Na kwa kuwa dhana hii ni ngeni na bado haijatambuliwa na wadau wakuu wa maendeleo ya nchi hii wakiwemo wanasiasa, wavuvi, wakulima na wafanyabiashara.

Je, ni lini Serikali itatoa mafunzo kwa wananchi yatakayohusiana na dhana nzima ya uchumi wa buluu.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

4. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Shehia ya Sizini iliyopo ndani ya jimbo la Wingwi imepata maji safi na salama miaka mingi tena bila ya kuwa na tangi la kuhifadhia maji.

Je, ni lini Serikali italijenga tangi la uhakika la kuhifadhia maji katika shehia hiyo.

50. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika kijiji cha Mjini Wingwi viko viwanda vinne (4) vya kusaga kokoto ambapo wananchi katika maeneo hayo hupata usumbufu sana wa kelele za mashine hizo pamoja na mavumbi yatokanayo na mashine hizo wakati wa zoezi la utengenezaji wa bidha hizo.

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuandaa mpango maalum wa kuwalipa fidia wananchi wanaoishi katika maeneo hayo yenye viwanda posho maalum kwa ajili ya usumbufu huo wanaoupata wa kiafya na kimazingira.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

56. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Eneo la Selem liliopo katika jimbo la Mfenesini ni eneo la Wizara ya Kilimo ambalo kwa muda mrefu limekuwa likitumika kwa kilimo cha mazao mbali mbali ikiwemo minazi, mihogo, ndizi na mazao ya muda mrefu. Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni eneo hilo wamepewa watu binafsi na kubakisha eneo dogo kwa Wizara ya Kilimo.

(a) Kwa kuwa Wizara imeshindwa kuendeleza eneo hilo na kwa kuwa katika ugawaji wa eneo hilo wananchi wa jimbo la Mfenesini hawakuingizwa katika mgao huo, na kwa kuwa wengi wa wananchi hao hawana sehemu za kulima wala kuishi. Je, Serikali ipo tayari kuwapatia angalau nusu eka kwa kila mmoja ili waweze kujikimu kiuchumi.

(b) Kwa kuwa Wizara haina wafanyakazi wa kutosha, hali inayopelekea kuibiwa kwa mazao mengi. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo hilo.

(c) Ni vigezo gani vilivyotumika katika kugawa eneo hilo kwa watu binafsi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

68. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Zanzibar ina eneo kubwa la bahari na sasa Serikali inaelekeza katika uchumi wa buluu ikiwa na nia ya kuzitumia fursa zilizopo baharini.

(a) Je, Serikali inachukuwa hatua gani kukiimarisha chama cha mabaharia Zanzibar ili kisaidie kuwapatia fursa wazanzibari.

(b) Ni fursa za aina gani chama cha mabaharia kinaweza kuzipata katika uchumi wa buluu.

(c) Je, chama cha mabaharia kama ni wadau wa shughuli za bahari, kinashirikishwaje katika mipango inayohusiana na usafiri wa bahari.

133. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha miundombinu ya barabara za ndani katika vijiji mbali mbali vya Zanzibar. Hata hivyo, kumekuwa na dhiki kubwa ya kusafirisha wagonjwa kwa kufuata matibabu kutoka Dodeani kwenda Finya, kutokana na ubovu wa barabara hiyo ya kilomita 6.5 ambayo imetolewa ahadi nyingi za viongozi kuitengeneza ikiwemo ahadi ya tripu 50 za kifusi zilizotolewa na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, Makamo wa Pili wa Rais mstaafu alipotembelea Dodeani kwa mara ya mwisho.

(a) Je, ni lini barabara hii ya kilomita 6.5 ya Dodeani-Finya itatengenezwa kama ilivyoahidiwa.

(b) Kwa vile barabara hii ni muhimu sana, Je, Serikali haioni haja ya kuitengeneza kwa kiwango cha lami badala ya fusi kama ilivyoahidiwa awali.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

108. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Chuo cha Kiislamu (CCK) Pemba kilichopo Micheweni kwa sasa kimegawiwa na kuwa chuo cha kufundishia walimu chini ya utegemezi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwepo skuli ya sekondari. Hata hivyo, bado zipo changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa mabweni ya kuishi wanafunzi na ikizingatiwa ni kando ya vijiji na kwa sasa baadhi ya wanafunzi wanaishi kwenye vyumba vya madarasa kwa nyakati za usiku.

(a) Ni mikakati gani ambayo Serikali imeshaanza kuichukua kuondosha changamoto hiyo.

(b) Na lini tatizo hilo linatarajiwa kuondoshwa katika chuo hicho na sekondari.

143. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Serikali imekuwa ikijitahidi kuboresha huduma za elimu kwa lengo la kuboresha maendeleo ya skuli za Unguja na Pemba. Hata hivyo, kumekuwa na kudhoofika kwa maendeleo ya baadhi ya skuli kwa sababu ya mabadiliko ya mara kwa mara ya walimu wakuu.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuhamisha walimu wakuu mara kwa mara kwenye skuli moja hakuleti matokeo mazuri kwa skuli husika.

(b) Je, ni sababu zipi zinazosababisha walimu wakuu kuhamishwa hamishwa pamoja na kwamba wanafanya vizuri katika skuli wanazoondolewa.

(c) Je, Serikali inatumia vigezo na mfumo gani wa kupeleka walimu wakuu kwenye skuli husika.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

103. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Katika utekelezaji wa programu ya kuendeleza utalii nchini, Wizara yako ilijipangia malengo na kuweka idadi ya wageni (watalii) watakaoingia nchini ili kuhakikisha kwamba pato linalotokana na utalii linaendelea kushika nafasi ya mwanzo katika kuchangia uchumi wa Zanzibar.

(a) Je, ni wageni (watalii) wangapi kulingana na daraja (class) zao waliotarajiwa kuingia nchini kwa kila kundi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha zimepatikana katika utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai – Septemba 2021/2022 kufuatana na daraja zilizopangwa.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

48. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Tatizo la ugonjwa wa mifupa (*Sickle Cell Disease*) limekuwa kubwa sana hapa Zanzibar. Na kwa kuwa dawa za maradhi haya zinapatikana katika hospital ya Mnazi Mmoja pekee.

Je, Serikali haioni kuwa iko haja ya kuandaa utaratibu mahsusi wa kuwapatia dawa hizo hospitali za Wilaya ili kuwaondolea usumbufu wagonjwa ambao hutakiwa kufuata dawa hizo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tu.

**Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

55. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Moja ya lengo kuu la Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 ni kuwapatia wananchi ardhi na makazi bora. Hivyo, mara tu baada ya kufanikiwa kwa Mapinduzi hayo, Rais wa kwanza na muasisi wa Mapinduzi hayo marehemu Abeid Amani Karume aliwagawia

wananchi eka tatu (3) ili waweze kufaidi matunda ya Mapinduzi hayo na kuwaondoa katika umasikini uliokithiri.

(a) Kwa kuwa muda mrefu umepita tangu kuchukuliwa kwa hatua hiyo, Je Serikali imeweza kufanya tathmini ya mafanikio ya lengo hilo.

(b) Ni ekari ngapi zimetolewa tangu uamuzi huo ulipofanyika na ngapi zimeshauzwa na kutumika kwa matumizi mengine.

(c) katika Wilaya ya Magharibi "A" wananchi waliokuwa wakiishi katika eka za watu wamefukuzwa ingawa wengi wameishi zaidi ya miaka 30 katika maeneo hayo. Je, Serikali ina kauli gani juu ya kadhia hii.

## III. <u>TAARIFA ZA SERIKALI:</u>

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:</u>**

Taarifa ya Serikali kuhusu mtumishi wa Serikali kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kupitia Kitengo cha Benki ya Damu.

**Zanzibar,**
**15 Septemba, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**